# UWAZI BAINA YA MASLAHI NA VIKWAZO

# الانفتاح بين المصالح والهواجس

**KIMEANDIKWA NA:**
**SHEIKH HASAN MUSA AL-SAFFAR**

**Kimetarjumiwa na:**

Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

# ترجمة

# الإنفتاح بين المصالح والهواجس

تأليف

حسن موسى الصفار

من اللغة العربية  إلى اللغة السواحلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN No: 978 – 9987 –17 – 041 – 8**

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Januari, 2014
Nakala: 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ........................................................................................ 01

Utangulizi........................................................................................................ 03

Klabu ya Awamiyah .......................................................................................... 03

Uwasilishaji wa Ustadh Husain Aal Nimri, Mwenyekiti wa semina................. 04

Uwazi, Ukuruba na Umoja, ni Anwani za Kiislamu za Asili............................. 08

Haki ya Ijtihadi na Uhalali wa Kutofautiana Katika Rai ................................... 14

Vipaumbele au Makubaliano?............................................................................. 18

Maswali naMichango ya Hadhira ....................................................................... 25

Mwishowa Semina............................................................................................. 46

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-Infitah bayna 'l-Masalih wa 'l-Hawajis* kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa al-Saffar. Sisi tumekiita, *Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo.*

Kitabu hiki kimetokana na semina zilizofanyika huko Awamiyah, Mkoa wa Qatif, Saudi Arabia. Lengo la semina hizo ni kuongeza maarifa na ujuzi wa waumini na pia kueneza moyo wa upendo licha ya kuwepo tofauti katika mitazamo ya kimadhehebu.

Sisi wachapishaji tunakiwasilisha kitabu hiki kama kilivyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo humo, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyoko ndani yake.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia, matusi, kashifa na kugombanishwa wenyewe kwa wenyewe ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyohiyo, imeamua kukichapisha kitabu hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu, hususan wanaozungumza Kiswahili.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki, Sheikh Hasan Musa al-Saffar kwa kazi kubwa aliyofanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu, Allah 'Azza wa Jallah, amlipe kila la kheri na amuingize

Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru Ndugu yetu Abdul Karim Juma Nkusui kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na yeye Allah Tabaraka wa Ta'ala, amlipe kila kheri hapa duniani na Akhera; pia bila kuwasahau wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mola wa viumbe. Eee Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad na Kizazi cha Muhammad kama ulivyomswalia Ibrahim na Kizazi cha Ibrahim, na mbariki Muhammad na Kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahimu na Kizazi cha Ibrahimu, hakika Wewe ni Mwenye kutukuzwa Mtukufu.

**Klabu ya Awamiyah:**

Klabu ya Awamiyah katika mji wa Awamiyah Mkoa wa Qatif, Wilaya ya Mashariki, imeanzishwa tarehe 30 /6 /1426Hijiria.

Klabu inafanya kikao mara moja kwa mwezi kila jioni ya siku ya Alhamisi ya mwisho ya kila mwezi wa Hijiria.

**Lengo la klabu:**Ni kukuza maarifa, kuainisha na kutoa ufumbuzi wa matatizo ya kijamii pamoja na kutia nguvu majadiliano yenye lengo, kupitia njia ya kueneza moyo wa upendo pamoja na kuwepo tofauti zakimitazamo. Wastani ndio mfumo ambao klabu imeufuata tangu kuasisiwa kwake, ambapo imechukua nembo yake katika aya tukufu:

وَكَذَٰلِكَ جَعَلۡنَٰكُمۡ أُمَّةٗ وَسَطٗا لِّتَكُونُواْ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيۡكُمۡ شَهِيدٗاۗ

**"Na kama hivyo tumewafanya kuwa ummah wa wastani, ili muwe mashahidi juu ya watu wote, na Mtume awe shahidi juu yenu."**

**(Surat al-Baqarah: 143)**.

**Machapisho:** Klabu imezingatia suala la kuimarisha semina zake kwa kuzitoa katika magazeti na tovuti, kisha ikaboresha kazi yake kwa kutoa vijitabu ambavyo vinakusanya semina zilizofanywa katika kozi za mwanzo za klabu ambazo zilikuwa zimetangulia na kuongoza katika kazi hii.

## UWASILISHAJI WA USTADH HUSAIN AAL NIMRI, MWENYEKITI WA SEMINA:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, swala na salamu zimwendee mbora wa Manabii na Mitume, Muhammad(saww) na Kizazi chake kitwaharifu, ama baad.

Ndugu mliohudhuria! Assalaam AlaikumWarahamatullahi Wabarakatuhu.

Tunaweza kusema kwamba semina zote na vikao vyote vya maarifa katika jamii yetu, na katika jamii zingine vilevile, katika harakati zake za maarifa mbalimbali, hugusa mazungumzo yanayoafikiana na anwani zake, kwa misamiati ambayo imeanza kuonekana kwa sura ya wazi kwa wenye macho katika wakati wetu huu, zaidi kuliko wakati wowote uliopita, kwa kutoa maana zake na kwa kutaja muonekano wake, kwa kusimulia mazuri yake na mabaya yake, na kadri ya kukubaliwa kwake na makundi ya jamii mbalimbali kwa kuchukua matokeo yake au kuyakataa kabisa.

Na misamiati hiyo kwa mfano tu na si yote, ni kama utandawazi, usasa na kuwa muwazi kwa wengine. Na kuhusu msamiati wa mwisho, kuna majadiliano makali. Joto lake limeongezeka baada

ya matukio ya tarehe kumi na moja Septemba, mjadala upokatika mvutano, kuna wanaosema hakuna haja ya kutilia maanani msamiati huo, kutokana na matokeo ambayo unaweza kutuachia, ikiwa ni pamoja na kutufanya tuache misingi yetu na itikadi yetu tukufu, na vile vile kutuvua utu wetu upande wa tabia njema na utamaduni. Na upande wa pili tunakuta kundi kubwa linaloelemea katika dharura ya kuchukua msamiati huo, na hususan katika wakati wetu huu, kwa kuzingatia kwamba dhana ya msamiati huo ni moja ya misingi ya fikira ya Kiislamu inayojengeka juu ya msingi wa tofauti kwa namna zake mbalimbali, nao ni msingi ulioenea katika ulimwengu. Zaidi ya hapo ni kwamba kuwa muwazi kwa wengine kunatuwezesha na kuturahisishia njia ya kufaidika na uzoefu wao na tajriba yao, na faida hii ni nguvu tunayoitumia kuelekea katika kiwango cha jamii zilizoendelea.

Na miongoni mwenu kuna kundi linalolingania kujenga umoja-na kuzalisha kila nguvu na juhudi ya watu wa ummah mmoja katika kazi ya kujenga na kuendelea kuelekea kwenye maendeleo yenye ustawi. Muadham Sheikh Hasan bin Musa as Safar Mwenyezi Mungu amhifadhi, amekuwa akitafakari na bado angali hivyo, kufanya kazi kwa kila alichopewa na Mwenyezi Mungu ikiwa ni pamoja na azma na bidii, ili kufanikisha lengo hili la kimaendeleo katika nyanja ya uwepo wetu, hivyo katika kila mnasaba kwa kudokeza au kwa kuelezea, haachi kuashiria umuhimu wa kuwa wazi kwa wengine, sawa iwe katika hafla ya kitaifa au ya kimataifa, au iwe katika magezeti au semina au katika vitabu vyake ambavyo miongoni mwavyo ni *al-Hiwar Wal-Infitaahi Alal-Aakhar* (Mazungumzo na Kuwa Muwazi kwa Wengine), na humo msomaji ataona katika anayoyasoma maelezo ya sababu za kukata mahusiano na ubaya wake, sababu zinazolingania kwenye majadiliano yenye kulenga kwenye malengo matukufu, baada ya kuorodhesha mazuri yake ambayo yanachangia katika kufanikisha kwake.

Kitabu chake hiki kimeshehe ni matokeo ya uzoefu aliohusika mwenyewe, nao ni mkutano wa kuleta ukaribu baina ya madhehebu uliofanyika Bahrain, na mkutano wa majadiliano ya kitaifa uliyofanyika Saudia. Na kutokana na kukinai kwake kwa dhati juu ya umuhimu wa maudhui, tunamuona anaondoa tatizo la wale wanaoona kuwa uhalali wa kufanya hivyo (kuwa muwazi kwa wengine), unapelekea kuachana na misingi thabiti ya madhehebu na ni kujivua maadili yake na misingi inayolingania, na kwamba hivyo viwili (yaani kuwa muwazi kwa mwingine, misingi na maadili ya madhehebu) ni sawa na vitu viwili vinavyopinga (hasi mbili) ambavyo haiwezekani kuvikusanya pamoja kulingana na istilahi ya wanamantiki.

Na kwa sababu sisi hapa, katika klabu ya Awamiyah hatuko katika kupendelea upande mmoja dhidi ya mwingine, na huwa hatuko - hivyo - tunapokuwa katika nafasi ambayo tunajaribu humo kuwakinaisha wahudhuriaji juu ya umuhimu wa matokeo ya maudhui yanayowasilishwa, mgeni wetu katika usiku huu mtukufu Sheikh Hasan as Safar, atakuwa ndio mzungumzaji katika wakati huu, wa yale yaliyojitokeza kwake miongoni mwa uzoefu wake na natija iliyopatikana baada ya matukio yote hayo na majadiliano ambayo ameyafanya katika madhumuni haya. Na msikilizaji mtukufu baada ya hapo anapasa kutoka na ukinaifu wake wa dhati ambao hatolaumiwa na yeyote juu yake, ikiwa ni pamoja na kuhifadhi mafungamano na mahusiano ya kibinadamu baina ya watu, mahusiano yaliyosalimika kutokana na kila ikhitilafu au mtengano, kwa sababu tu ya rai katika maudhui haya au yale.

# MUHADHARA[1]

Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Shetani mwenye kulaaniwa.

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Asalaamu Alaykum Warahamatullahi Wabarakatuhu.

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, swala na salamu zimwendee Mwisho wa Manabii na Mitume, Nabii wetu Muhammad, Kizazi chake kitwaharifu na Masahaba wake wema, ama baada.

Naanza kwa kuelezea furaha yangu ya kuwepo kwangu katika klabu ya Awamiyah, klabu hii ambayo nimefuatilia uanzishwaji wake na nimefuatilia habari zake zenye kufurahisha kwa kuizingatia kuwa ni taa kati ya taa za fikira na maarifa.

Ndugu zangu! Mazungumzo yetu usiku huu ni juu ya uwazi, na nimegawa mazungumzo yangu katika nukta kuu tatu, nazo ni:

1. Uwazi, ukuruba na umoja, ni anwani za Kiislamu za asili,

2. Haki ya ijtihadi na uhalali wa kutofautiana katika rai,

3. Ni vipaumbele au makubaliano?

[1] Ni semina iliyofanywa na klabu ya Awamiyah usiku wa Jumatano tarehe 25 Rabiul-Awal 1429 Hijiria, sawa na 3 April 2008, kwa anwani ya Uwazi Baina ya Uangalifu na Kuhifadhi Turathi.

# NUKTA YA KWANZA:

## UWAZI, UKURUBA NA UMOJA NI ANWANI ZA KIISLAMU ZA ASILI

Hakuna shaka kwamba kujitokeza kwa maudhui yoyote ile huwa ni kwa sababu ya kuhitajika kwa maudhui ya anwani hiyo, au kwa sababu kuna kundi au upande unaoamini anwani hiyo na unakwenda mbio kuitoa na kuidhihirisha. Hiyo ni kwa sababu katika fikira na utamaduni wa Kiislamu kuna anwani nyingi, lakini baadhi yake zinachukua mwelekeo wake na upeo wake katika nafasi ya kujitokeza na kudhihiri, wakati ambapo nyingine zinaweza kuwa zimefichikana au zimefifiana hazijajitokeza. Na wakati anwani hizi zinapojitokeza zinaweza kukabiliana na baadhi ya alama za maswali kwa sababu ya mkanganyiko wa hali ya maisha.

Na sisi tunakuta anwani mfano wa maudhui ya Haki za Binadamu, ambayo Mwislamu hawezi kupinga kwamba asili yake ni ya Kiislamu, na wala mtu hawezi akadai kwamba sio ya Kiislamu au kwamba Uislamu haulinganii kuheshimu na kulinda Haki za Binadamu, tunaona maudhui haya yalipungua katika jamii ya Kiislamu na yalijitokeza maudhui mengine kwa sababu ya mazingira ya kisiasa. Na mukabala wa mazungumzo kuhusu Haki za Binadamu, kulikuwa na msisitizo na mkazo juu ya Haki za Mwenyezi Mungu Mtukufu, au juu ya haki za viongozi, au haki za maulamaa na mfano wa hao. Hivyo makundi maalum katika jamii– kwa sababu ya nafasi zao za kijamii- yalikuwa yakiziteka anwani hizi, na mazungumzo kuhusu heshima yao na haki zao yalikuwa yakijitokeza bayana wazi wazi.

Ama mazungumzo kuhusu Haki za Binadamu kama binadamu, yalikuwa ni anwani iliyofifia, na ndivyo ilivyokuwa kuhusiana na mazungumzo juu ya Haki za Mwanamke, nayo vilevile yalikuwa ni anwani iliyofifia kwa sababu ya hali ya mazingira ya kimaarifa na kijamii ambayo ummah ulikuwa unaishi nayo.

**Umoja Baina ya Asili na Kutoweka:**

Na miongoni mwa anwani hizo ni: Uwazi, ukuruba na umoja baina ya watu wa ummah mmoja, nazo ni miongoni mwa anwani za Kiislamu za asili, ambazo hatuhitaji mazungumzo ya ziada juu yake ili kuwasilisha na kutoa hoja na dalili inayothibitisha asili yake katika fikira na utamaduni wa Kiislamu. Lakini sisi tunakiri kwamba mazingira ambayo ummah wetu uliishi yamefanya anwani hizi kuwa katika kivuli.

Hata wakati zinapowasilishwa, anwani hizi zinaonekana kana kwamba ni ngeni na zinaleta mashaka, na kana kwamba zinahitaji uthibitisho, ambapo yanaulizwa maswali mengi juu yake na inatolewa mishkeli na shaka nyingi juu yake, na hili ni jambo la kushangaza, kana kwamba asili ni ubinafsi, ugomvi na mfarakano wa kimadhehebu, na hivyo anayelingania uwazi au ukuruba ni lazima alete dalili na hoja, na hivyo ni wajibu kwake kuhalalisha msimamo wake.

Kana kwamba kugawanyika ummah na kuparaganyika katika makundi ndio hali ambayo inapasa iimarishwe. Na anayelingania umoja na ukuruba anakuwa chanzo cha dhihaka na istihizai. Na hii yenyewe kwa hakika ni dalili inayoonesha kiwango cha kina cha upotovu ambao sehemu kubwa ya watu wa ummah inaishi nao, na upo katika sehemu kubwa ya jamii zetu, na sisi hatuna haja ya kuthibitisha anwani hizi, kwani kuna aya nyingi tukufu ambazo wote wamezihifadhi, zinazothibitisha anwani hizo, kati ya hizo ni kauli yake (swt):

وَٱعْتَصِمُوا۟ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا۟ ۚ ﴿١٠٣﴾

**"Na Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane."** **(Surat Imran: 103)**.

Na kauli yake (swt):

إِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَٰحِدَةً وَأَنَا۠ رَبُّكُمْ فَٱعْبُدُونِ ﴿٩٢﴾

**"Hakika ummah wenu huu ni ummah mmoja, na mimi ni Mola Wenu kwa hivyo niabuduni." (Surat Anbiyai: 92).**

Na kauli yake (swt):

وَإِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَٰحِدَةً وَأَنَا۠ رَبُّكُمْ فَٱتَّقُونِ ﴿٥٢﴾

**"Na hakika ummah wenu huu ni ummah mmoja na Mimi ni Mola Wenu, basi nicheni." (Surat Muuminun: 52).**

Na kauli yake (swt):

وَأَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَا تَنَٰزَعُوا۟ فَتَفْشَلُوا۟ وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ وَٱصْبِرُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ

**"Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wala msizozane, msije mkavunjika moyo na zikapotea nguvu zenu, na subirini; Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri." (Surat An'faal: 46)**.

Na zaidi ya hapo ni Hadithi na riwaya ambazo zinalingania kwenye uwazi, ukuruba na umoja. Na nususi hizi za kisharia zinatia mkazo kwamba uwazi ni asili katika uhusiano baina wa binadamu,

vyovyote zitakavyotofautiana dini, achilia mbali madhehebu, madrasa na rai. Hivyo anwani hizi ni maudhui za Kiislamu za asili. Zaidi ya hapo ni kwamba akili inamtaka mwanadamu atekeleze maudhui haya katika maisha yake ya kivitendo na ya kila siku, nayo ni kwa maslahi yake kama mtu binafsi, na kwa maslahi yake kama jamii, na ni kwa maslahi yake kama taifa.

Zaidi ya hapo kuna lengo la ujumbe. Ikiwa mwanadamu ni mwenye kujali dini yake na ni mwenye ikhilasi katika madhehebu yake, hakika kujali kwake na ikhilasi yake kwa ajili ya itikadi yake vina mlazimisha kufikiria fursa itakayomwezesha kusambaza itikadi hiina kuielezea kwa wengine kwa njia nzuri. Na hali hii haitotimia kwa kujitenga na kujifungia, wala haipatikani katika mazingira ya mizozo na ugomvi. Lakini inawezekana mtu kueleza dini yake na itikadi yake kwa njia salama na nzuri katika mazingira ya kujuana na uelewano, na kwa sababu hii hakika Qur'aniTukufu inahesabu kujuana kuwa ni msingi wa ubinadamu, anasema (swt):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَـٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَـٰكُمْ شُعُوبًا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓا۟ ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ
عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

**"Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari." (Hujurat: 13)**.

Na pengine swali linaweza kuulizwa: Ni nani anayehutubiwa katika wito wa umoja, ukaribu na uwazi? – Maelekezo haya yanaelekezwa kwa kila Mwislamu mwelewa kwa kiasi cha uelewa wake, na hususan maulamaa, wasomi na walinganiaji, hawa wanaelezwa na Mwenyezi Mungu kwamba wabebe jukumu hili muhimu na kazi hii.

Hapa ni lazima kutokee maswali ya kujiuliza kuhusu maulamaa na wasomi ambao wanakaa na kuzembea kulingania umoja na ukuruba, ambapo ilipasa tuulize:Kwa nini mwanachuoni huyu halinganii umoja? Na kwa nini mwanachuoni huyu haendi mbio kuleta ukuruba pamoja na madhehebu mengine? Tunawataka hawa kutoa sababu za misimamo yao ya kizembe, na sio sahihi kuwepo maswali kuhusu anayelingania ukaribu na umoja. Sisi tukiwagawa maulamaa makundi mawili, tutakuta kuna kundi linalojali maudhui haya na kupeperusha bendera hii, na kuna kundi jingine halitaabishi nafsi katika kushughulikia jambo hili. Hakika katika hali ya uelewa salama na sahihi, ni juu ya watu kuwahukumu maulamaa na wasomi wanaozembea kulingania kwenye umoja na wasiotaka kwenda mbio kuleta ukuruba, na wawaambie:Kwa nini hamjafanya harakati zozote (za kuleta umoja)?Na mmefanya nini katika nyanja hii?

Na hususan ummah, nchi na makundi yanapoishi katika hali ya kuzingirwa na hatari ya fitina za mgawanyiko, hapa inapasa watu wawaulize na wawahukumu hawa maulamaa, kwa nini hawajabeba jukumu lao katika kuutetea msingi kati ya misingi ya dini, na kushikamana na sehemu ya wito wa msingi wa Qur'ani, nao ni msingi wa Umoja baina ya Waislamu. Ni wajibu waelekeze maswali kwaona wawahukumu kwa kuzembea kwao, na waulizwe sababu ya wao kutofanya kazi hii ya kiungu.

Na inasikitisha sana kusikia – kwa baadhi ya watu – mazungumzo ya kuleta ukuruba na umoja kwa aina ya dhihaka, istihizai na dharau, na hususan wakati yanapotokea baadhi ya matukio au misimamo ya kundi fulani, ambapo kuna wanaodharau kwa kusema: Huu ndio umoja! Na huu ndio ukuruba!Kwa maana kwamba maudhui ya umoja na ukuruba yamekuwa yanazungumziwa kwa aina ya dharau na kejeli, na hapa sina jingine isipokuwa kutaja kauli yake (swt):

وَلَا تَتَّخِذُوٓا۟ ءَايَـٰتِ ٱللَّهِ هُزُوًا ۚ ﴿٢٣١﴾

**"Wala msizifanyie mzaha Aya za Mwenyezi Mungu."**
**(Surat al-Baqarah: 231)**.

Na hiyo ni kwa sababu huu ni msingi uliyomo ndani ya Qur'ani, lakini kuna wanaoudhihaki, wanaudharau na kuubeza, wakati ambapo ni wajibu kuudharau msimamo mwingine ambao haufuati mfumo huu wa Qur'ani, na sio tuchukue ubaya wa hali ya nje kisha tuwabebeshe ubaya huo walinganiaji wa umoja.

Ukuruba na umoja unazuia kutendeana ubaya, lakini ubaya unaopatikana katika baadhi ya nyakati hausababishwi na kitendo cha kulingania kwenye umoja bali ni kwa sababu ya hali maalum. Na wala haipasi lawama hizi zinazotokana na baadhi ya makosa yanayofanywa katika jamii ya Kiislamu, kuzielekeza kwenye hatua zinazolenga kuleta ukuruba, jambo ambalo hupelekea baadhi ya watu kudharau hatua hizi. Je tunapasa kuidharau Swala eti kwa sababu tu kuna mtu ambaye Swala yake haimzuii kufanya machafu na maovu? Hii si sahihi. Kwa sababu hiyo ni wajibu wetu kushutumu madai haya na hali hii ambayo inatengenezwa dhidi ya walinganiaji wa ukuruba na umoja, kiasi kwamba wanatazamwa kwa dharau kana kwamba wao wanawajibika na matukio haya, wakati ambapo ukweli ni kwamba wanakabiliana na kazi nzito iliyoangukia katika mgongo wa ummah.

# NUKTA YA PILI

## HAKI YA IJTIHADI NA UHALALI WA KUTOFAUTIANA KATIKA RAI

Katika historia ya maarifa ya Kiislamu kuna mapambano ya tangu zamani baina ya wahafidhina ambao huwa na hofu, shaka na mashaka mbele ya rai yoyote nyingine au mabadiliko na maendeleo yoyote. Kuna aina hii ya maulamaa na wenye kushughulika katika nyanja ya maarifa katika historia ya ummah. Na aina nyingine ni ile ya walio huru kutokana na hofu hii, ambao wanatumia haki yao katika ijtihadi na kutoa rai hata kama inakhalifu mazoea na inapingana na rai mashuhuri.

Hakika ni mapambano ya zamani na mapya, na mazungumzo hivi sasa ni kuhusu uwazi na ukuruba na ndio unaoangazia mwanga wake juu ya vita hivi. Hivyo vita vya uhuru wa kutoa rai ni moja ya muonekano wa mapambano haya, hiyo ni kwa sababu mwelekeo wa wahafidhina unataka kukumbatia sharia. Ni kana kwamba wanayoyasema na kuyajengea ndio asili na ndio sharia, na kwamba wanaotoa rai nyingine yenye kukhalifu ile ambayo imeenea na ambayo ni mashuhuri katika dini yao, basi hao dini yao ina shaka, na wanawatuhumu kwa bidaa na upotovu na mfano wa hayo. Mapambano haya ni ya tangu zamani na mas'ala haya hayafungamani na kazi ya kisiasa.

Baadhi ya watu – kama tunavyosoma katika baadhi ya maandiko – wanachochea hofu hii kwa madai kwamba, haya ni madai yanayofanya kazi kwa malengo na maslahi ya kisiasa, wakati ambapo

ukweli ni kwamba mas'ala yametokea ndani ya mapambano haya baina ya mielekeo hii miwili, nayo ni ya kina na ya zamani kuliko jambo hili. Katika historia yetu kuna maulamaa wengi ambao walikuwa na ijtihadi yenye kukhalifu rai iliyoenea. Kuwepo na ijtihadi nyingi –sawa iwe katika mas'ala ya kiitikadi au mas'ala ya kifiqhi au mas'ala ya kihistoria – ilikuwa ni jambo linalokubalika. Kwa mfano, Sheikh Suduq (r.m) naye ni kati ya waasisi wa elimu na fikira katika madhehebu ya Ja'fariyah (Shia Ithnaashariya) – Faslu ya mambo ya kiimani - baada yake alikuja mwanafunzi wake Sheikh al-Mufid (r.m) akaandika mas'ala ambayo alimjibu Sheikh wake katika kitabu alichokiita *Tasihihul-Itiqaadi* (Masahihisho katika Itikadi), katika kitabu hicho alimkhalifu Sheikh Suduq katika mas'ala 43 ya kitheiolojia, na kitabu hicho kimechapishwa na ni maarufu.[2] Lakini kuna baadhi ya watu na baadhi ya shakhsiya wanafanya haraka kuwatuhumu wale wanaowakhalifu katika rai wakati ambapo historia yetu imejaa mfano wa mambo kama haya.

Na imepatikana katika historia yetu mengi kati ya matukio mabaya ambayo yanawezekana kuwa chini ya anwani ya Ugaidi wa Kifikira, nalo ni jambo linaloendelea hadi katika zama hizi vilevile, ambapo tunakuta mfano wa hali hii. Huyu hapa Imamu Khomeini (r.m) alikuwa anaumia katika moja ya hotuba zake kwa yale yaliyomkabili- kulingana na maelezo yake – kutoka kwa wale waliojifanya watakasifu, wasioendelea na waliokwama, kutokana na shida ambazo zilimpata kutoka kwao. Imamu alikuwa anawatambua kama watu wasioendelea, waliokwama na kwamba wao ni wenye kujionyesha kuwa ni watakasifu. Na - kwa sababu ya Imam kushajiisha na kufundisha kwake falsafa – jambo hili liliwafikisha katika hali ambayo mtoto wake Mustafa Khomeini alikuwa anapokwenda kwenye Seminari ya al-Faidhiya na kunywa maji katika gilasi, wanafun-

[2] Vitabu viwili vimechapishwa katika mjaladi mmoja kitika silsila ya utunzi wa Sheikh al-Mufid, mjaladi wa tano, chapa ya pili 1414 Hijiria Darul-Mufid, Beirut –Lebanon.

zi wengine na masheikh wao walikuwa hawanywi kwa gilasi hiyo hadi waitwaharishe kwa sababu tu amenywea gilasi hiyo mtoto wa mtu anayefundisha falsafa katika Seminari ya Masomo ya Kidini, hali ilifikia kiasi hiki.

Imamu ametumia ibara kali na ngumu kukabiliana na hali ya hawa wenye kujitukuza na kujifanya watakasifu. Anasema alipokuwa analihutubia Bunge: "Hakika baadhi ya wasiotaka maendeleo wenye kujifanya watakasifu wanaona kila kituni haramu, na hakuna yeyote anayeweza kusimama dhidi yao. Hakika uchungu alioumeza baba yenu mzee kutoka kwa hawa wasiotaka mabadiliko ni uchungu ambao hajaumeza kamwe kutoka kwenye mashinikizo na matatizo mengine yote."[3] – Yaani Imamu Khomeini anaweka yote aliyokabiliana nayo kutoka katika utawala wa Shah, siasa ya Marekani na mashinikizo ya mabeberu wa kimataifa katika mkono mmoja wa mizani, na anaweka mashinikizo ya hawa wasiotaka mabadiliko wanaojidhihirisha kwa utakasifu katika mkono mwingine wa mizani.

Hakika ninayotaka kutanabahisha katika nukta hii ni kwamba kuna makundi mawili katika kila jamii, katika yale yanayohusiana na jambo la kidini na kifikira, na kuna uwezekano kila kundi hutoa rai yake na mtazamo wake lakini linapasa– katika mukabala wa hayo – kuruhusu wengine kutoa rai zao, na vilevile kudhihirisha rai yake kuhusu ile rai wanayoitoa wengine, lakini bila ya kukimbilia kwenye Ugaidi wa Kifikira kwa kutilia shaka dini ya upande mwingine na kuutoa katika madhehebu, na kuuelezea kama upande ulioritadi, uliopotea na wenye bidaa na mfano wa hayo. Na bila kukimbilia kuvuka mpaka, kumlenga mtu binafsi, kuchafua heshima za watu

[3] Al-Bahraaniy: Ja'fari Shaakhuriy, katika *al-Harakiyatual –Aqiliy al-Ijtihaadiy Ladaa Fuqahaai Shiati al-Imamiyati*, uk: 10, Chapa ya Kwanza 1419 Hijiria Darul-Mulaak – Beirut, kutoka katika *Sahifati Nuuri*, Juz. 21, uk: 19.

wenye kuheshimika, na kutenda lile ambalo haliendani na uhuru wa kifikira, eti tu kwa sababu ya kutofautiana naye katika rai. Haipasi mambo kama hayo kuenea katika jamii, nayo ni hali mbaya, na wala haisaidii katika kukuza fikira na maarifa katika jamii hii na kwa watu wake.

# NUKTA YA TATU

## VIPAUMBELE AU MAKUBALIANO?

Mara nyingi baadhi ya watu hawa huchochea mambo kwa kudai kwamba walinganiaji wa umoja huachana na itikadi, misingi na kaulimbiu (za dini au madhehebu) kwa ajili ya kuleta ukuruba na upande mwingine na kupata upendo wake. Na hapa ni wajibu tuseme – kwa uwazi kabisa – kwamba, hatupaswi kuwashughulisha watu kwa maudhui ambazo zinatekenyana kuamsha hisia zao na hamasa zao. Mbele yetu kuna uzoefu kutoka katika kundi la kisalafi (Mawahabi) la ndugu zetu Masunni, namna gani wenye misimamo mikali katika kundi hili wametumia mfano wa mbinu na anwani hizi kwa ajili ya kulazimisha ukaidi wao na Ugaidi wao wa Kifikira katika medani.

Na sisi – kama wafuasi wa Ahlulbayt (as) - tumekabiliana sana na mengi miongoni mwa ukali huu, ukaidi huu na Ugaidi huu wa Kifikira ambao unafanywa na Masalafi (Mawahabi) wenye msimamo mkali dhidi ya Shia na dhidi ya wenye kuwakhalifu katika rai, na wala haisihi abadani kukubali kutumia njia hii katika madhehebu yetu.

Na mimi sioni tofauti baina ya Salafi(Wahabi) wa Kisunni mwenye msimamo mkali anayewatuhumu Shia kwa bidaa na shirki kwa sababu tu wao wanawakhalifu katika rai, na baina ya Shia mwenye msimamo mkali anayemtuhumu kuwa amepotea na ni mwana bidaa yule mwenye kumkhalifu katika rai ndani ya duara la Ushia. Njia na mfumo ni huo huo, nao haukubaliki hata uwe unatoka kwa nani. Na

misingi kwetu iko juu ya watu, na hakuna umaasumu kwa yeyote, sisi tunamheshimu faqihi kwa ajili ya fiqhi yake, na tunaheshimu nafasi yake, lakini misingi hatuwezi kuivuka wala hatuwezi kumfanya yeyote awe juu ya misingi hiyo. Na wakati tunapozungumza kuhusu rai na mielekeo tunasema, rai hii ni ya makosa na mfumo huu ni wa makosa, bila ya kutia shaka katika dini ya yeyote au katika utakasifu wa mtu, bali tunamhesabu ni mtu aliyetumia njia na mfumo usio sahihi katika nyanja hii.

Na kwa sababu hiyo ni juu yetu, kwanza: Tutofautishe ni yapi yaliyo misingi na ni yapi ambayo ni itikadi pindi tunapo tofautiana katika rai kuhusu ufafanuzi au tawi kati ya matawi ya itikadi. Kwa sababu suala sio 'wewe achia au endelea kushikilia lakini mimi sijakinaika kwamba mas'ala haya ni katika itikadi,'suala si kuacha itikadi lakini suala ni kutofautiana katika mfano halisi wa itikadi husika.[4]Ni katika kuainisha je jambo hili ni katika itikadi au hapana? Haisihi abadani kutumia dalili ya jumla na anwani ya jumla katika shaka inayohusu mfano halisi. Kwa mfano, mimi naafikiana na wewekatika wajibu wa kujiepusha na najisi, lakini naweza kutofautiana na wewe kwamba hiki kitu ninachokiona nje ni najisi au sio najisi? Wewe huwezi kunihukumu kwamba mimi napuuzia najisi, kwanza njoo unikinaishe kwamba hii ni najisi, na baada ya hapo nituhumu kwamba mimi napuuzia najisi.

Pili: Kuna baadhi ya mambo yanaweza kuwa ni katika itikadi nani katika sharia, lakini kuna mazingira yanayopelekea kuyavuka mambo haya au kuyaacha bila kuyatekeleza, kwa sababu kuna

[4] Kwa mfano tu Waislamu wote wanajua na wanaitakidi Mungu ni Mmoja na ni Yeye tu wa kuabudiwa na kwamba Shirki ni haramu, lakini Mawahabi kwa ufinyu wao wa maarifa wanaona mtu kuzuru kaburi la walii yeyote ni kumshirikisha Mungu, hivyo kwa maoni yao finyu kuzuru kaburi ni mfano halisi wa Shirki, wakati ambapo kwa maoni ya Waislamu wengine kuzuru kaburi si mfano halisi wa Shirki. Hivyo hapa suala lenye utata si uharamu wa Shirki bali utata ni je kitendo hiki cha kuzuru kaburi ni Shirki ili kiwe haramu? - **Mhariri.**

kipaumbele muhimu zaidi. Uwezekano huu upo, nani anaweza kuthibitisha bila ya shaka kwamba haisihi kuacha jambo lolote katika dini? Katika baadhi ya nyakati inasihi kuacha jambo fulani bali katika baadhi ya hali ni lazima kuacha. Kwa nini basi mnaelekeza mapanga kwa watu kwa kuwatishia watu kwa mapanga hayo? Huyu hapa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ameacha jambo alipoona kwamba maslahi yapo katika kuacha na akakubali kufuta '*Bismillah*' na neno '**Mtume wa Mwenyezi Mungu**' katika Mkataba ambao aliuandika pamoja na washirikina wa Kikuraishi.

Vinapokea vitabu vya sira kwamba yeye (saww) alimwambia Ali (as) katika suluhu ya Hudaibiya: "Andika: Bismillahi Rahman Rahim," Suhail, mwakilishi wa watu wa Makka akasema: "Ama *Rahman* sijui ni nini, lakini andika *Bismika Allahummah*"Waislamu wakasema: "Wallahi hatuandiki isipokuwa: *Bismillahi Rahman Rahim*."Nabii (saww) akasema: "Andika *Bismika Allahummah*. Haya ndio mambo aliyokubaliana Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)" Suhail akasema: "Kama tungejua kwamba wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu tusingekuzuia kufikaNyumba Tukufu wala tusingekupiga vita, lakini andika Muhammad bin Abdillahi." Nabii (saww) akasema: "Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu hata kama watanikadhibisha." Kisha akamwambia Ali: "Futa 'Mtume wa Mwenyezi Mungu.'" Akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika mkono wangu hauwezi kufuta jina lako katika utume." Mtume wa Mwenyezi Mungu akaushika mkono wake akafuta. Kisha akamwambia Ali, andika: "Haya ndio mambo aliyokubaliana Muhammad bin Abdillahi na Suhail bin Amru …."[5]

[5] Al- Majilisiy: Sheikh Muhammad Baaqir katika *Biharul- An'war*, Juz. 20, uk. 333 Daul-Ihiyaai turath al-Arabiy chapa ya tatu 1403 Hijiria, na al-Bukhariy: Muhammad bin Ismail katika *Sahihul- Bukhari* Juz. 2, uk. 200, mlango unaozungumzia masharti ya Jihadi na kufanya sulhu na Makafiri maadui, na kuandika masharti, Hadith namba 2731 Darull- kutubi 1420 Hijiria Beirut.

Makuraishi walipinga na hawakukubali kuweka ibara ya *Bismillahi* kama wanavyoitumia Waislamu, ambapo waliizingatia kuwa ni nembo ya Kiislamu na wakamtaka Nabii (saww)aandike ibara nyingine watakayoafikiana juu yake. Na pia walikataa ibara ya "Mtume wa Mwenyezi Mungu" kwani kama wangekuwa wanaitakidi utume wake, basi wasingempiga vita kulingana na maneno yao, na Nabii (saww) alitosheka kwa kuandika jina lake tu na ibara '*Bismika Allahummah*.'Nalo ni jambo lililopelekea baadhi ya Masahaba kupinga na kuchukia - kama ilivyotangulia – ambapo walizingatia kufanya hivyo ni kuacha itikadi, lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mwenye akili na hekima akaamuru kufuta '*Bismillahi*' na neno 'Mtume wa Mwenyezi Mungu'na akasema (saww): "Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu hata kama watanikadhibisha." Yaani hata kama watanikadhibisha washirikina, yaani hakuacha kwa kukinai bali aliacha kwa ajili ya maslahi.

Ni wajibu tuulizane: Tukio hili linaelezea nini? Je, halielezei juu ya maslahi katika maudhui ambayo yamepelekea uongozi mkuu wa Kiislamu, ambao unawakilishwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu kuachwa kwa ajiliya maslahi ya juu zaidi? Na jambo hilo hilo tunalikuta kwa Amirul-Muuminina Ali bin Abi Talib (as), japo alikuwa anaamini kwamba Uimamu na uongozi ni haki yake lakini yeye alisalimisha na akaacha jambo kwa Makhalifa, na yeye ndiye mwenye kusema: "Wallahi nitasalimisha maadamu mambo ya Waislamu yako salama na ikiwa humo hakuna dhulma isipokuwa kwangu tu."[6]Na katika sehemu nyingine anasema: "Nikazuia mkono wangu hadi nikaona kurejea kwa watu, wameshatoka katika Uislamu wanalingania kufuta dini ya Muhammad(saww). Nikaogopa kama sintounusuru Uislamu na watu wake, basi nitaona humo pengo au mvunjiko, na msiba wake kwangu utakuwa ni mkubwa zaidi kuliko kupoteza

[6] *Nahjul-Balaghah*: Miongoni mwa maneno yake (as) walipo azimia kumpa Bayi'a Athman.

uongozi wenu ambao kwa hakika ni raha ya siku chache. Yanaondoka kwayo yale yaliyokuwepo kama yanavyoondoka mazigaziga au kama yanavyoondoka mawingu. Nikaamka katika matukio hayo hadi ikaondoka batili na kutoweka, na dini ikapata matumaini na kuhifadhika."[7]

Lakini hii haimaanishi kwamba aliacha kwa kutoamini kwamba yeye ndiye mwenye haki. Bali katika uhalisia wa kivitendo alikuwa chini ya Makhalifa waliokuwepo madarakani, na aliamiliana pamoja nao kwa msingi huu, na hiyo ni kwa sababuya maslahi.

Na vivyo hivyo wakati tunaposoma sira ya Imam Hasan bin Ali (as) tunamkuta anaacha utawala na uongozi kwa Muawiya bin Abi Sufian. Maimamu waliobakia (as) vilevile walikuwa wanaacha kwa dhahiri, ni sawa katika misimamo yao ya jumla au katika maelezo ya kimatendo waliyoyatoa kwa anwani ya *Taqiya*, nayo ni anwani ambayo mafaqihi wameitafiti na hatimaye wakaigawa katika aina mbili:

*Taqiya*ya kuepuka madhara na *Taqiya* ya kuleta maelewano - kama alivyoiita Sayyid Khui – au kama walivyoiita mafaqihi wengine *Taqiya* ya kuleta upendo.

Taqiya ya kuepuka madhara katika hali ya kuhofia kupatwa na madhara, ni anwani wazi na ni ya kiakili. Ni kawaida mtu asidhihirishe imani yake au kutenda wadhifa wake wa kisharia kwa ajili ya kuhifadhi maslahi yake au kujikinga na madhara ambayo yanaweza kumpata katika hali ya kutekeleza amali hii yenye kumdhuru. Hii niTaqiya ya kuepuka madhara na kujikinga na madhara.

Ama Taqiya ya kuleta maelewano katika muamala au Taqiya ya kuleta upendo, mafaqihi wanakusudia kwamba mtu asidhihirishe

---

[7] *Nahjul-Balaghah*, katika barua yake kwa watu wa Misri pamoja na Maliki al-Ashtar alipompa ugavana na uongozi wa Misri.

imani yake au kutenda wadhifa wake wa kisharia, sio kwa kuhofia madhara bali ni kwa ajili ya kuuvutia upande mwingine na kupata mahaba yake. Mfano wa wazi wa aina mbili hizi za Taqiya ni: Kuswali pamoja na ndugu zetu Masunni. Sisi- katika madhehebu ya Ahlulbayt tunatofautiana na ndugu zetu Masunni katika baadhi ya ufafanuzi wa hukumu za Swala, lakini mafaqihi wetu wanatoa fatwa kwamba tunapokuwa katika sehemu ambazo humo wanapatikana baadhi ya ndugu zetu Masunni, ni mustahabu kwetu tuswali pamoja nao kama wanavyoswali wao, na hilo linapendeza kwao. Ama katika hali ya uwezekano wa kutokea madhara ni wajibu kwetu tuswali pamoja nao. Katika hali ya kwanza wanaiita Taqiya ya kuleta maelewano katika muamala, au Taqiya ya kuleta upendo, kwa sababu hii ni kwa ajili ya kujenga muamala na mahusiano mazuri na upande mwingine, wakati ambapo nyingine wanaiitaTaqiya ya lazima.

Na hali ni hiyo hiyo katika sehemu yoyote ile ambayo yanapatikana humo matatizo ya kusujudu juu ya kinachosihi kusujudu juu yake au kutofunga mikono. Sharia haiamuru kuswali kulingana na maelezo ambayo wanatoa maulamaa wetu katika fatwa zetu, na hii sio kuacha imani yetu, hapa kuna kulinda imani na rai, kwani kamakutokutenda kwa mujibu wa imani yetu kuna maslahi zaidi kushinda kudhihirisha imani yetu au kutenda kwa mujibu wa imani yetu, maslahi kama vile kuhifadhi umoja wa ummah au kuleta upendo kwa ndugu zetu Waislamu, hapo sharia na fiqhi inapendekeza kuacha kutenda kwa mujibu wa imani yetu, na hii ni fatwa iliyotolewa na mafaqihi wetu.

Na hapa nanukuu fatwa ya Sayyid Khui katika *Swiratun-Najaat,*[8] *naye ni muwazi sana katika nyanja hii, nayo ni mas'ala namba 515 katika juzuu ya kwanza ukurasa wa 157, ambapo swali linasema: Nini makusudio ya Taqiya katika ibada na je inawezekana kuiin-*

[8] Cha ya kwanza 1425, Maktbatu Fadak – Qum – Iran.

*giza katika hukumu tano,*[9] *na je huwa sehemu ambayo kunadhana ya kukhofia madhara au wakati wa kujipendekeza kwa muonekano na kutokujali?*

*Sayyid Khui akajibu kwa kauli yake: "Ama katika sehemu ambayo kuna uwezekano wa kupata madhara kwa kuikhalifu (Taqiyah) ni wajibu, na katika kuswali pamoja nao ni mustahabu iwapo hakuna dhana ya kuwepo madhara."*

*Na hapa (kwa mujibu wa Sayyid Khui) hata kama hakuna madhara ni mustahabu kuswali pamoja nao.*

*Hakika anayeita anwani hizi kuwa ni kuacha itikadi, katika baadhi ya nyakati huwa ima haelewi madhumuni yake na upeo wake, au ni kwamba makusudio yake ni kuwasahaulisha watu na kutekenya hisia zao na mawazo yao. Hapa tunahitimisha mazungumzo kwa nukta tatu:*

**Nukta ya kwanza:** Hakika kulingania uwazi, ukuruba na umoja ni wajibu wa Kiislamu wa kisharia, na ni juu ya jamii kumwajibisha anayekhalifu na asiyetekeleza wajibu huu.

**Nukta ya pili:** Ijtihadi na uhalali wa kuhitalifiana ni msingi ulioafikiwa. Sio haki kwa yeyote kutuhumu rai ya mwingine kwa kumshutumu kuwa ametoka na ameasi dini kwa sababu hiyo, hii ni kinyume na maadili na dini, na ni kinyume na mfumo wa kielimu, na kuhitalifiana katika rai kupo tangu utamaduni wa madhehebu ya Ahlulbayt ulipoanza.

**Nukta ya tatu:** Inapasa – kwanza – kutofautisha na kuainisha sehemu zenye tofauti, je hii ni katika itikadi na sharia au hapana? Kisha baada ya hapo ndipo tuzungumze, je jambo hili linapaswa kuachwa au halipaswi kuachwa? Na upande wa pili wa nukta hii ni kwamba: Hakuna kizuizi

[9] Wajibu, Mustahabu, Haramu, Makuruhu na Mubahu –**Mhariri**.

cha kuacha muonekano wa kivitendo wakati kunapokuwepo na maslahi matukufu zaidi, na panapokuwepo na vipaumbele.

Swali linalobakia ni: Ni nani anayeainisha hayo? Najibu swali hili kwamba anayeainisha hayo ni wale wenye kushughulika na jukumu hili kama ilivyo katika sekta nyingine zozote. Tunaposema kwamba Zaka wanapewa mafakiri, ni nani mafakiri? SioMarjaa ndiye anayeainisha fulani ni fakiri na fulani sio fakiri bali ni upande unaohusika, kama vile jumuiya za kujitolea ambazo hufanya kazi ya kutafiti hali ya mwenye kudai kuwa yeye ni fakiri, na kwa msingi wake zinaainisha ufakiri au utajiri wake, kama ilivyo katika maudhui nyingine ambazo ni upande unaohusika unaofaa na wenye kutegemewa ndio huainisha maudhui husika.

# MASWALI NA MICHANGO YA HADHIRA

**Adil Aal Ibrahim:**

Muadham Sheikh!Je, huoni kwamba baadhi ya tofauti zinarejea katika mambo ya kinafsi kwa daraja la kwanza katika tabia ya jamii, na hiyo ni kwa sababu ya kiburi na kujikweza, kiasi kwamba kunapatikana hali ya kukata udugu baina ya wanafamilia na wanandugu licha ya wao kuwa ni watu wa karibu kabisa?

**Sheikh Safar:**

Mimi naafikiana na wewe katika rai, kwa sababu baadhi ya tofauti – huenda sehemu kubwa miongoni mwazo – zinatokana na mazingira kama hayo, vinginevyo sisi hatukuti kwamba kutofautiana katika dini au madhehebu au rai kuwa ni sababu ya kutengana na kukata mahusiano, Qur'aniTukufu katika aya iliyowazi dhahiri shahiri inasema:

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي ٱلْكِتَٰبِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَقْعُدُوا۟ مَعَهُمْ
حَتَّىٰ يَخُوضُوا۟ فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِۦٓ ﴿١٤٠﴾

**"Na amekwisha wateremshia katika Kitabu hiki kwamba mtakaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na kuchezewa shere, basi msikae pamoja nao mpaka waingie katika mazungumzo mengine." (Surat Nisaa: 140).**

Yaani ni kwamba hakuna kizuizi cha Mwislamu kukaa katika kikao cha makafiri, lakini anapowasikia wanamkanusha Mwenyezi Mungu anawaacha katika wakati huu hadi waingie katika mazungumzo mengine. Na haipatikani kwetu sharia inayoruhusu kukata mahusiano nao isipokuwa katika baadhi ya hali, kunapokuwepo na

uovu au bidaa iliyo nje ya dini, na haisihi kuhesabu tofauti inayopatikana katika ijtihadi kuwa ni bidaa. Ndio, kuwatenga watu waovu na wanabidaa ambao wanaingiza katika dini yasiyo kuwemo - ikiwa kuwatenga ni sababu ya kusaidia kuwaonya- ni sahihi, ama wakivuka hatua hii kiasi kwamba jamii au baadhi ya jamaa zao ikiwatenga au wasipomtenga, bado hawatobadilisha kitu, hapa hakuna sababu ya kuwatenga.

Ama kuhusu hali ya kinafsi ya kuhusudiana, ya kiburi na kujihisi udhaifu, hili ni jambo linalopatikana na linasikitisha. Kuna baadhi ya watu hawapendi kuwasiliana na wewe kwa sababu tu anapokuona anahisi udhaifu wake na wala hajiamini katika kuamiliana na wewe, hivyo anaiweka nafsi yake mbali kutokana na kitishofulani. Hakika anajihisi udhaifu ambao unamfanya asikutane na wewe, vinginevyo mwanadamu ambaye anaiamini nafsi yake, hakika anakutana na wengine hata kama anatofautianavyovyote vile, nao wanatofautiana naye. Lakini pamoja na masikitiko makubwa tunakuta hali hii isiyo ya kimaendeleo ndio inayowapelekea baadhi ya watu kufuata njia ya kutengana na kuvunja mahusiano, kwa sababu tu yeye anatofautiana na upande huu au ule katika rai yake au msimamo wake.

**Ali Dabiysiy:**

Tunamkaribisha Sheikh katika klabu ya Awamiyah. Napenda kuchangia hapa baadhi ya fikira na maswali kuhusu fikira za muhadhara huu, Sheikh anasema: "Kwamba maudhui ya uwazi katika fikira ya Kiislamu na katika vitendo vya Kiislamu imekataliwa sana, kama zilivyokataliwa anwani zinazofanana nayo, mimi - hapa namkhalifu Sheikh katika ujumla, na hiyo ni kwa kuitakidi kwangu kwamba mara nyingi zinakataliwa namna na si anwani, vinginevyo anwani hizi ni za msingi kama ulivyosema, lakini namna ndizo zilizokuwa kitovu cha tofauti na mizozo.

Na mazungumzo yanapokuwa ni kutoka kwa Sheikh Hasan Safar, basi hakuna njia ya kuzuia kuzungumzia harakati za Sheikh Hasan Safar na kuulizana juu yake, na kama angekuwa ni mzungumzaji tu na mtoa nadharia tu basi katika mazungumzo yetu tungekomea katika nadharia ambayo ameitoa. Lakini mzungumzaji (ambaye ni Sheikh Safar) anatoa nadharia na wakati huo huo inafungamana na harakati maalum anazozifanya Sheikh, hivyo ni lazima Sheikh aturuhusu sisi kwamba katika michango yetu kuwepo pia na yale yanayohusu harakati zake. Sheikh anatumbukia katika maeneo ya uwazi, hivyo hufunguka na huwa muwazi hapa nchini kwa namna makhususi, na kuna rai ambazo haziafikiani na hali ya ndani, hivyo hakuna kizuizi cha kuwa muwazi.

Umoja ndio anwani ambayo inaweza kumuogopesha mwingine- vile vile, Sheikh amezungumza na ameashiria kwamba upande mwingine unatumia baadhi ya njia ambazo ni wajibu tusizitumie, hivyo basi hata njia ya kuwaogopesha wengine kwa anwani ya umoja haikubaliki vilevile, kwa sababu umoja sio hatua ya mwanzo daima katika mfumo wa maadili, siku moja unaweza kuwa wa mwisho, na siku nyingine unaweza kuwa kabla ya hapo, na inawezekana usiwepo kabisa kutokana na baadhi ya sababu, hata aya ambayo daima tunaitumia kama ushahidi wa kuhimiza umoja:

وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُواْۚ ﴿١٠٣﴾

**"Na Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane."** **(Sura Imran: 103)**, iko wazi sana, kushikamana ni katika kamba ya Mwenyezi Mungu, hivyo inapokosekana kamba au pakushikwa na upande mwingine, hapa panaweza kuwepo na umoja usiolingana na uhalisia wa aya tukufu.

Nukta nyingine ni katika vipaumbele vya makubaliano: Bila shaka wanaomfuatilia Sheikh wanajua kwamba rai za kiitikadi katika miaka kumi na tatu ya mwisho hazikuwepo na haya ni mambo mapya ambayo hayakuwepo mwanzo. Na hii ni rai yangu na inaweza kuwa ni ya makosa, sisi tumeona kwamba zimetokana na kambi za kisiasa zaidi kuliko kuwa zimetokana na mtazamo wa kiitikadi. Kwa dalili kwamba zimepatikana sasa ndani ya mfumo huu wakisiasa, na mfano ambao ameutoa Muadham Sheikh kama ushahidi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifuta *Bismillahi*, hapana shaka ni ndani ya upinzani maalum. Nadhani kwamba mfano huu ni mzuri sana na muhimu sana katika mtiririko wa mazungumzo ya Sheikh ili kwa mfano huo tutoke na kwenda kwenye kauli ya kwamba, hapana shaka aliyefuta *Bismillah* ni Mtume wa sharia, na ni kawaida kwamba kuacha sharia katika sharia ni wajibu kufanywe na mtu anayesimamia mambo ya sharia katika nafasi ya kwanza, na hivyo ni ima awe ni mtu mwenye uwezo wa kifiqhi au anafungamana na faqihi.

Mwisho Sheikh amewasilisha anwani ya wenye kushughulika na mambo, nayo ni mas'ala yanayohitaji uchambuzi vilevile, ni wenye kushughulika katika anwani yoyote ya tawi? Au wenye kushughulika kwa ujumla? Au wenye kushughulika katika daraja maalumla fiqhi? Wenye kushughulika – peke yake bila sharti lolote – ni anwani isiyofaa kushughulikia mambo ya kiitikadi katika kipengele cha kuwa muwazi kwa wengine, inapasa wenye kushughulika wawe wametimiza anwani nyingine ambazo hapana shaka kwamba Sheikh anazijua zaidi.

**Sheikh Safar:**

Mchango mzuri, ama kuhusu nukta ya kwanza: Kwamba hakika wale ambao wanakataa hawakatai anwani bali wanakataa namna. Mimi natamani wawe hivyo, na tofauti katika jambo ni kwamba

anayekataa namna hakika yeye anatoa badili na namna nyingine. Baadhi ya Waislamu walipoongolea Haki za Binadamu na wakasema Uislamu hauko dhidi ya Haki za Binadamu lakini sisi kama Waislamu haturidhishwi na baadhi ya vipengele katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, swali waliloulizwa lilikuwa ni: "Nini badili ambayo mnaipendekeza?" Na hatimaye vikapatikana vikao na mikutano kadhaa, na katika mikutano hiyo ikapendekezwa mikakati kwa jina la Azimio la Kiislamu laHaki za Binadamu, na vile vipengele visivyoridhisha vikafanyiwa kazi.

Na mimi nasema ikiwa kukataa ni kwa sababu ya namna, je hawa maulamaa wana mkakati mwingine kuhusu umoja na ukuruba? Je, wamejitahidi kukutana na wengine? Je, wamefanya harakati yoyote katika upande huu? Je wamekabiliana na wamelingania katika upande huu? Kama ingekuwa hivyo katika mfumo maalum tungesema: Hawa wana matatizo katika namna na hawana tatizo lolote katika anwani, lakini tatizo ni kwamba utakuta kuna kujitenga na mwelekeo huu. Mimi nimesoma maandiko na nimesikia baadhi ya hotuba zinazungumzia umoja kwa dharau na istihizai. Ikiwa baadhi wana tatizo katika namna, basi haisihi kwa mtu huyo kudharau asili ya anwani au asili ya mwelekeo, bali ni juu yake kuijadili namna maalum na ajitahidi kupendekeza namna mbadala. Hii ni katika yanayohusiana na nukta ya kwanza.

Ama nukta ya pili ambayo ameizungumzia ndugu yangu: Kwamba ni harakati ya kijamii na kwamba hizi anwani zimedhihiri katika kipindi cha mwisho, katika baadhi ya rai za kiitikadina hususan katika mkakati wangu na mwelekeo wangu wa kijamii na wa kisiasa ninaouwasilisha. Pamoja na yakini niliyonayo, lakini kwa kadiri niwezavyo ni kwamba mimi siwasilishi kitu katika upande wa kiitikadi, na namuomba ndugu yangu alete mfano unaohusu mambo mapya ya kiitikadi ambayo nimeyawasilisha.

Labda kama ataihesabu rai yangu kuhusu kujikata (*twatibir*) kuwa ni rai ya kiitikadi! Mimi naitakidi hio sio rai ya kiitikadi. Au labda kama ataihesabu rai yangu kuhusu kufanya istikhara kwa tasbihi na Qur'ani kuwa ni jambo la kiitikadi! Mafaqihi hawajathibitisha kuwa kwake mustahabu kama inavyodhihiri katika fatwa ya Sheikh Tabriziy ambapo anasema: "Haijathibiti kuwa kufanya istikhara ni mustahabu."[10] Na vilevile Sayyid Sistaniy ambaye anasema: "Inafanywa kwa kutaraji thawabu wakati wa tahayari."[11]

Hivyo mimi sijawasilisha rai ya kiitikadi, bali nimewasilisha baadhi ya matatizo kwa kuwa ni matatizo ya kijamii, au kwa kuwa ni hali maalum ya kijamii ambayo nimeona ni dharura kuishughulikia na kupendekeza rai kuhusiana nayo. Nayo sio jambo la kiitikadi ninalohamasisha au ninalowasilisha, pamoja na kwamba nalinda haki yangu katika kueleza imani yangu, hususan ukizingatia kwamba mambo ya kiitikadi hayarejei katika taklidi.

**Ustadh Ali Dabiysiy:**

Samahani kwa kukukatisha, mimi nawashukuru wasimamizi wa semina kwamba wanatoa fursa ya kuchangia baada ya kuuliza swali, miongoni mwa rai za kiitikadi kama ilivyo wazi na maarufu kwa wote ni suala la kutukana Masahaba, yaliyomo humo na yanayolizunguka suala hilo. Na suala lingine - ingawa linazungukwa na rai za kifiqhi lakini lina asili ya kiitikadi - nalo ni suala la kuainisha uhusiano na Marjaa, kwa maana kwamba suala hilo linashughulikiwa ndani ya rai za kifiqhi na katika utangulizi wa utatifi wa kifiqhi, lakini kama tunavyojua lina uhusiano na Maimamu kumi na wawili (as) na lina aina fulani ya mafungamano na mas'ala ya kiitikadi, na

10 Al-Khui: Abul-Qasim al-Musawaiy pamoja na maelezo ya Sheikh Jawadi Tabriziy katika *Swiratwa Najatu Fiy Ajuwibati al-Istiftaati*, Juz. 1, Mas'ala namba 1534, uk. 553, Chapa ya 2 ya 1416 Hijiria, Maktabatul- Fiqihiya- Kuwait.

11 Sistaniy: Sayyid Ali al-Husainiy katika *Fiqihi lil-Mughitaribiina*, Mas'ala 598, uk. 344, Daru Kumail Bahrain.

hili huenda ni moja kati ya mas'ala ya kiitikadi, nalo ni eneo la ikhitilafu katika nchi yetu.

**Sheikh Hasan Safar:**

Mifano hii ambayo umeitaja nayo pia sio ya kiitikadi, mas'ala ya kutukana na kulaani sio katika mas'ala ya kiitikadi, wala hakuna yeyote anayeyahesabu hivyo. *Al-Baraatu* maana yake ni ujiepushe na maadui wa Ahlulbayt na waliowadhulumu, nako ni kujiepusha kwa moyo, na hili ndio kongamano la Shia. Ama kutukana na kulaani – hata kama kuna maneno juu yake – bado kwenyewe kunatokana na suala la ziyarat hii (inayowalaani madhalimu) kuwa mustahabu, au kunatokana na nususi zile (zinazowalaani madhalimu). Na kulingana na maalumati yangu na maarifa yangu suala hilo (la kulaani na kutukana) sio suala la kiitikadi.

Imamu Ali (as) anasema - katika wanayoyataja Shia: "Baada yangu atadhihiri juu yenu mtu mwenye koo pana, mwenye tumbo kubwa, anakula anachokipata na anatafuta asiyoyapata, basi muuweni (mkiweza), na wala hamtomuuwa. Ee hakika atawaamuru kunitukana mimi na kujiepusha na mimi. Ama matusi, nitukaneni kwani ku fanya hivyo ni utakaso kwangu na ni kuokoka kwenu. Ama kujiepusha na mimi msijiepushe na mimi."[12] Na mimi natoa changamoto, ijapokuwa baadhi ya watu neno changamoto linawaogopesha, mimi natoa changamoto kwamba mtu aniletee fatwa ya Marjaa kuhusu hali ya mazingira wanayoishi nayo Shia, amuulize, je inajuzu kwetu kutukana na kulaani? Mimi naomba fatwa moja tu kutoka kwa Marjaa anayesema: "Inajuzu au ni mustahabu." Nakaribia kusema kwamba kuna kongamano baina ya Marjaa juu ya kwamba, hili (la kutukana na kulaani) linamadhara, na kwamba haisihi na kwamba haijuzu. Na

[12] *Nahjul-Balaghah*: Anapowaambia Masahaba zake na akiwapa habari kuhusu mtu atakayewaamuru kumtukana.

yeyote apendaye kubisha basi Marjaa wapo, na maneno ya Sayyid Sistaniy ambaye ni Marjaa mkuu wa Mashia, maneno aliyoyatoa tarehe 14 Muharram 1428 Hijiria katika mnasaba wa kumbukumbu ya tukio la Samrau yalikuwa wazi bayana yakikataza kusema kila kinachosababisha mfarakano na kuchochea chuki.

Anasema: "Wote wanajua - na hali ndio hii – haja iliyopo ya kuunganisha safu na kupuuza mfarakano na kuwa mbali na sababu za ukabila, na kujiepusha kuchochea ikhitilafu za kimadhehebu, ikhitilafu hizo ambazo zimepitwa na karne nyingi. Na yaonyesha njia ya kuziondoa ni kwa yale yanayoridhiwa na yanayokubaliwa na wote, hivyo haipasi kuchochea mjadala kuhusu ikhitilafu hizo nje ya duara la utafiti safi wa kielimu. Na hasa ukizingatia kuwa hazigusi misingi ya dini na nguzo za itikadi, kwani hakika wote wanamwamini Mwenyezi Mungu mmoja tu Mpweke, ujumbe wa Nabii al-Mustafaa (saww) na marejeo, na kwamba Qur'aniTukufu - ambayo imehifadhiwa na Mwenyezi Mungu kutokana na upotovu- pamoja na Sunna tukufu ya Nabii ndio rejea ya hukumu za sharia, na kuwapenda Ahlulbayt (as), na mfano wa hayo miongoni mwa mambo ambayo yanawakutanisha pamojaWaislamu wote, na kati ya hayo ni misingi ya Uislamu: Swala, Saumu, Hija na mengineyo.

Haya ya ushirikiano ndio msingi wa sawa wa umoja wa Kiislamu, hivyo ni lazima kutilia mkazo juu yake ili kuimarisha mafungamano ya ummah huu. Na kwa uchache kabisa ni kuishi kwa salama baina yao (Waislamu) kwa misingi ya kuheshimiana, mbali na ugomvi na misuguano ya kimadhehebu na kikabila vyovyote itakavyokuwa anwani yake."[13] Maelezo haya yapo katika tovuti ya Sistani na yamenukuliwa katika magazeti na vyombo vya habari.

[13] www.sistani.org

Na natofautiana pamoja na wewe kwamba rai hizi ni rai mpya zilizoletwa na medani ya kisiasa. Kama tutasoma tutakuta kwamba rai hizi zina mizizi kwa maulamaa, mafaqihi na watafiti wa kishia tangu zamani, na sio maoni mapya, lakini hizi rai zilikuwa zimezuiliwa, na wahusika wa alama za umoja, ukuruba na uwazi walikuwa hawajatafutwa, na sira yaoilikuwa haijahuishwa kwa kiwango kinachotakiwa ndani ya jamii ya Kishia. Sayyid Burjurdiy aliyekuwa Marjaa mkuu katika zama zake, naye ndiye mwasisi wa Seminari ya Elimu ya Dini ya Qum, na hakuna yeyote asiyejua nafasi yake, kama utasoma maneno yake katika mas'ala ya umoja na ukuruba na kuunga kwake mkono uanzishwaji wa kituo cha *Daru Taqriybu Bainal Madhahibil-Islamiyah* huko Cairo, utashangaa namna gani shakhsiya hii na rai ambazo alizitoa imekuwaje zimezuiliwa na kufichwa. Vilevile mtu mfano wa Sayyid Muhammad Taqiy al-Hakim, Sheikh Kashiful-Ghitwaa ambaye alijitolea kupambana na uchochezi ambao ulikuwa unajitokeza huko Najaf Tukufu katika siku ya tisa ya mwezi wa Rabiu kwa jina la Iddi ya Zahraa, na akahutubia hotuba mashuhuri katika uwanja wa al-Alawiyya, na akatoa fatwa ya kuzuia na akawalingania watu kuwapiga vita hawa wajinga ambao wanahuisha vitu hivi, na haya yametajwa katika kitabu chake *Janatul-Maawaa*.[14] Na Sheikh hakuwa anaongoza chama cha kisiasa.

Na vilevile Sayyid Abdul-Husain Sharaf Diyn unaposoma kitabu chake*al-Fusulu al-Muhimatu Fiy Tauhidil-Ummah*na unaposoma *al-Murajaati* utakuta fikira zilezile. Na hii ni dalili kwamba mfano wa maoni haya yalikuwapo na yapo na sio jambo jipya lililoletwa na siasa mpya.

Nukta ya mwisho: Nani anayeshughulika? Na kwamba mafaqihi wao ndio wanaoshughulika na mas'ala haya, hapa nataka niashirie nukta mbili:

[14] Al-Kaashiful- Ghitwaa: Sheikh Muhammad Husain katika*Janatul-Maawaa*, uk. 170, Chapa ya kwanza 1380 Hijiria, Chapa ya Sharikatu Jaab, Tabriz – Iran.

**Nukta ya kwanza:** Hakika rai hizi ni fatwa za mafaqihi, lakini suala sio aliyesema mas'ala haya ni faqihi au si faqihi, suala ni kupambana na rai nyingine. Nani anashaka na weledi wa Sayyid Muhsin al-Amin al-A'miliy, mwandishi wa *A'yaan Shiah,* ni nani ana shaka naye katika kuwatetea Mashia na Ushia? Sayyid Muhsin al-Amin al-A'miliy ndiye mwandishi wa kitabu *Kashful-Iritiyaab*, na kitabu*al-Majalisi al-Husainiyati*, na vitabu vingine vingi. Ni nani anashaka na ikhilasi yake katika itikadi? Naye ndiye mwenye kitabu *Tan'zihuFiy A'amaali Shubhati*. Na vilevile Imamu Khomeini, Sayyid Khamenei, Sheikh Makaarim Shiraziy na Sheikh Muhammad Taqiy Bahjatiy. Hivyo suala sio aliyesema mas'ala haya ni faqihi au si faqihi.

**Nukta ya pili:** Kuhusu wenye kushughulika, nasema: Hakika anwani za Kiislamu, fatwa na hukumu za kisharia, upande wa utekelezaji wake katika maudhui unafungamana na mukalaf. Faqihi yeye humwambia mukalafu, ikiwa kuna tatizo au ugumu, na ikiwa kuna maslahi ya jamii, fanya kadhaa na kadhaa, anwani hizi hutajwa na mafaqihi, lakini ni nani anayeainisha? Na wao hapa hawajatoa sharti kwamba anayefanya kazi ya kuainisha maudhui ni lazima awe ni faqihi, au ni faqihi ndiye aainishe utekelezaji wake wa nje. Na dalili juu ya hilo ni haya tunayoyaona sasa, kwamba pande za kisiasa zinazoshughulika huko Iraki au Lebanon au katika medani nyingine mbalimbli za Kiislamu zinachukua maamuzi yake ya kisiasa zenyewe, licha ya kwamba zenyewe hazina nafasi ya kifaqihi na ijtihadi. Ndio, baadhi ya nyakati tunakuta wao wakirejea kwa Marjaa, na Marjaa huwaambia nyinyi kusanyikeni na amueni wenyewe, na jambo hili sisi tumeishi nalo pamoja na Marjaa Sayyid Shiraziy (r.m), tulipokuwa tunarejea kwake katika baadhi ya mambo ambayo yanafungamana na nchi alikuwa anatuambia: "Nyinyi ndio upande unaoshughulika, kusanyikeni na wenzenu na amueni." Hivyo wenye kushughulika na mambo ya nje ni wale am-

bao wanajua utekelezaji wake, na watu waliopo katika ardhi ndio wanaojua mambo ya jamii zao na mambo ya uhusiano wao pamoja na mazingira yanayowazunguka katika upande wowote wa kielimu na wa kifiqhi. Hiyo ni kwa sababu – pande za kifiqhi (Marjaa) - hazimiliki vyombo vya kutosha vya kuweza kuwafikishia taarifa na maalumati (sahihi). Marjaa hawajui ghaibu, na wala hawateremshiwi wahyi kutoka mbinguni ili kuwapa habari, wala hawamiliki vyombo kamili kwa sababu ya mazingira ambayo wanaishi nayo, na kwa sababu ya hali tunayoijua za Seminari zetu za Masomo ya Dini na za Marjaa wetu.

Na kama hali ilivyo katika Husainiyati na misikiti, mafaqihi hawaingilii humo, watu wanaiendesha na wanaongoza mambo yake. Na vivyo hivyo jumuiya za kheri na shughuli za kielimu, ambaye anataka kutunga kitabu haambiwi achukue rai ya Marjaa katika kitabu hiki au fikira ile. Na vilevile katika kiwango cha harakati za siasa na uhusiano pamoja na pande zingine. Ndio, ikiwa kuna jambo linalopingana na anwani inayohitajia hukumu ya msingi, hili ni jambo jingine, lakini maadamu mas'ala yako katika duara la anwani na hukumu, utekelezaji katika maudhui na uainishwaji wake ni mambo yameachwa kwa pande zinazohusika.

Nashangaa inakuwaje ndugu yangu anaashiria kwamba uhusiano pamoja na Marjaa na nafasi ya Marjaa ni katika mas'ala ya kiitikadi. Jambo la taqlid sio jambo la kiitikadi, bali ni njia ya kiakili tu, hata mafaqihi wanapojadili dalili ya wajibu wa kufanya taqlid, kuwa je ni ya kiakili au ni ya kisharia au ni ya kunukuu, wanasema dalili yake, ni dalili ya kiakili, na dalili ya kisharia ni ya mwongozo tu. Na hiyo ni kwa kuzingatia kwamba asiyejua anapasa kurejea kwa mwenye kujua, sasa inakuwaje unalifanya hili kuwa ni katika aina ya mambo ya kiitikadi?

**Abdallah Ali Aal Qariyriys:**

Muadham Sheikh tulijifunza kwenu wakati tukiwa wadogo, kutenda kulingana na uhalisia hata kama mazingira yatakuwaje, je mna nasaha inayohusu kuendelea katika jukumu la ujumbe mbele ya makundi yaliyokanganyikiwa? Shukran.

**Sheikh Safar:**

Nasaha katika upande huu tunaweza kuzungumzia katika nukta tatu:

**Nukta ya kwanza:** Kunyanyuka kwa uelewa na maarifa, na hili ni jambola dharura, kila utakaponyanyuka ujuzi wa mwanadamu na maarifa yake, basi atakuwa ni mwenye uwezo zaidi wa kutekeleza jukumu lake la kidini na ujumbe.

**Nukta ya pili:** Ni kushirikiana pamoja na wengine. Mwanadamu anapofanya kazi peke yake natija yake inakuwa ndogo na chache, hivyo ni lazima kushirikiana katika kazi ya uboreshaji na ya kijamii.

**Nukta ya tatu:** Uhusiano mzuri na kuamiliana pamoja na wengine, kwa sababu tabia njema ndio uso wa mwanadamu muumini, nayo ndio anwani ya ukurasa wa muumini kama ilivyopokelewa katika Hadithi na nususi.

**Amjad al-Faraj:**

Tunajua kwamba umoja na uwazi ni maana za zamani na za asili, na imetokea mikutano baina ya maulamaa zamani huko Cairo katika AzharTukufu, baina ya Maulamaa wa Azhar, Qum na Najaf, lakini tunakuta kwamba juhudi zinazotolewa katika mwelekeo huu daima hazileti mafanikio baina ya Maulamaa. Na uwazi na umoja haimaanishi kufuta madhehebu kwa madhehebu nyingine, lakini ni kuleta ukaribu na kuishi kwa maelewano. Kwa nini basi maelekezo hayawi baina ya Maulamaa wa madhehebu na wananchi (wa kawaida) au watu kutoka katika madhehebu mengine? Tunakuta kwamba juhu-

di zilizotolewa katika kujenga uhusiano baina ya Maulamaa katika mwelekeo huu hazikuleta natija kubwa, kutokana na sababu ambazo mojawapo inaweza kuwa ni ile uliyoitaja ya kuhisi udhaifu mbele ya upande mwingine. Lakini tunakuta uzoefu mfano wa Hizbullah na uzoefu wa Iran katika upande wa siasa, umeweza kuwavutia wananchi wa dola zingine ambazo zinafuata madhehebu mengine, ndio kunapatikana mihadhara ya Kiislamu na semina, lakini bila malengo.

**Sheikh Safar:**

Ahsante. Mimi nakuafiki katika rai kwamba kulingania tu katika umoja na ukuruba hili – peke yake – halitoshi, ni lazima kuwepo na ratiba ya kazi katika ardhi na baina ya watu wenyewe, haya ni maneno salama na sahihi. Na kuhusu hali yetu katika nchi yetu, mimi nawalingania watu waingize upande wa pili katika jambo na wala kadhia isiwe kana kwamba ni baina ya maulamaa tu au baina ya makundi fulani. Wasomi na viongozi wa jamii ni wajibu wawe na nafasi. Inapasa tujihadhari na hali ya mustakbali wa mazingira katika nchi yetu na katika sehemu yetu ya ghuba kwa ujumla, kutokana na mwanga wa yale ambayo tunayaona katika nchi zingine. Na kisha ni wajibu wetu tulinde umoja na tulinde hali katika nchi zetu kwa ziada ya kuamiliana vizuri na kukaribiana kwa kiwango cha watu na jamii. Ni lazima– kwa mfano tu – kuwe na maingiliano mazuri katika klabu za utamaduni, katika kazi za ushirikiano nakatika kazi za kijamii. Ni lazima twende mbio katika mwelekeo huu, na mimi natamani wafuasi wa Ahlulbayt (as) wawe kama walivyotakiwa na Ahlulbayt (as). Sisi tunataka kufikisha ujumbe wa Ahlulbayt (as) kwa ajili hiyo ni lazima tuwe na miradi ya kibinadamu ya jumla na manufaa kwa watu wote. Na katika nyanja hii ni kwa nini basi haitimii kazi ya kuanzisha miradi ya kibinadamu au vituo vya utafiti na masomo kwa kiwango cha kitaifa? Au hospitali kwa ajili ya kutibu magonjwa sugu kwa kiwango cha kitaifa au kanda?

Au makazi ya kujitolea kwa ajili ya mafakiri? Au kazi ya kushajiisha utafutaji elimu na kusoma masomo ya juu kwa kiwango cha taifa na kanda?

Kama mfanyakazi ambaye ni Shia katika kanda ya Mashariki atachangia kutoka katika mfuko wake katika miradi elfu moja, nusu ikiwa ni ya watoto wa kisunni na nusu yake ni yawatoto wa kishia, hilo litakuwa na athari kubwa zaidi katika kulingania umoja, na hii ni katika kusadikisha Hadithi: "Kuweni walinganiaji kwa nafsi zenu bila ya kutumia ndimi zetu, na kuweni pambo letu na wala msiwe dosari kwetu."[15] Na itakuwa ndio uso wa madhehebu yetu badala ya kutosheka tu na kujenga Husainiya na kukaa kusoma majilisi na kufanya maatamu humo. Nalo ni jambo muhimu, mimi sidharau Husainiya na kusoma majilisi, lakini je huu tu ndio wajibu wetu? Je, Imamu Hasan (as) alipokuwa anabeba viroba juu ya mgongo wake kila usiku na kutoa sadaka, je alikuwa na orodha ya nyumba za Mashia tu na hivyo alikuwa anawapelekea sadaka wao tu? Au alikuwa anampa kila mwenye njaa na kila fakiri na kila mtu?

**Ali Aal Saif:**

Kwa kuzingatia kwamba kuwa muwazi kwa wengine na kufanya majadiliano na wengine kunaathiri juu ya uhusiano wa Mwislamu na Mwislamu, na Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu katika msingi wa mwafaka, inawezekana nikaafikiana pamoja na ndugu yangu Mwislamu katika jambo ambalo kimsingi mimi natofautina naye, lakini kwa njia ya mwafaka naweza kulifumbia macho, lakini mwafaka huu unaweza kunitoa katika mfumo wangu na itikadi yangu ya msingi na kunisababishia matatizo yanayonitoa katika duara la Uislamu, je ka-

[15] Al-Kullainiy: Muhammad bin Yaaqub katika *al-Kaafiy*, Juz. 7, uk. 77, Hadith 9, Mwaka 1985 Darul-Adhuwaai – Beirut.

tika kufanya mwafaka na upande mwingine kuna mpaka maalumu unaotakiwa kuheshimiwa na upande mwingine kiasi kwamba hakika upande wa pili hautakiwi kuuvuka kwa sababu atakuwa ametoka nje ya duara maalum? Kama nitakutana na mtu Mhindi na akaniambia: Dini yenu ni dini ya kujifunga na hairuhusu uwazi kwa wengine, na kama utamuuliza juu ya dalili huenda atakwambia: Hakika nyinyi hamturuhusu sisi kwenda Makka kwa ajili ya kuzuru sehemu zenu takatifu, na sisi haturuhusiwi kuingia Msikiti Mtukufu na Msikiti wa Mtume, na pia anapoingia yeyote katika dini yenu ili kuijua hawezi kutoka ndani ya dini yenu. Na anaelekeza ukosoaji kwa kuzingatia kwamba hii ni sehemu ya uwazi, nini litakuwa jibu lako kwa swali hili?

**Sheikh Safar:**

Narejea kwenye anwani ambayo umeitoa katika swali lako: Je, kuna mpaka katika kufanya mwafaka au hakuna?Katika kiwango cha kiitikadi hakuna yeyote anayetaka kwako kuacha itikadi yako na wala haisihi kwako hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

مَن كَفَرَ بِٱللَّهِ مِنۢ بَعۡدِ إِيمَٰنِهِۦٓ إِلَّا مَنۡ أُكۡرِهَ وَقَلۡبُهُۥ مُطۡمَئِنُّۢ بِٱلۡإِيمَٰنِ ﴿١٠٦﴾

**"Anayemkufuru Mwenyezi Mungu baada ya imani yake, isipokuwa aliyelazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya imani."**

**(Surat Nahli: 106)**.

Itikadi iko ndani ya moyo na haitakiwi kuiacha katika jambo lolote bila ya kukinai kwako, na wala haisihi wala haiwezekani kuacha itikadi, kukinai kwako na mambo ambayo unayaamini kwa uhakika, hivyo hakuna mwafaka katika duara la itikadi. Itikadi ambayo inafungamana na viungo vyako, hii haina nafasi ya mwafaka,

wala hakuna yeyote anayekwambia uache fikira au itikadi au rai, niwajibu kwako kushikamana na itikadi yako ambayo unamwamini Mwenyezi Mungu kwayo.

Nukta ya pili: Nayo nikuhusu vitendo vya nje, sisi hatuna Taqiya katika damu na utupu, hivyo haijuzu kufanya Taqiya ambayo itapelekea kumuuwa yeyote au kuvunja heshima ya mwanamke, hii haisihi. Ama katika yasiyokuwa hayo katika vitendo vya nje, humo kuna nafasi pana ya Taqiya, hata katika kiwango cha kuacha Swala na kuacha Saumu na kuacha Hija na kuacha faradhi yoyote kati ya faradhi, ikiwa tu kuitekeleza kwake kunasababisha hatari katika maisha yako au afya yako, hapo hakika inajuzu kwako kuiacha. Na baada ya hapo utailipa kadha ikiwa ni katika yale ambayo ni wajibu kulipa kadha. Hivyo mwafaka ni katika mpaka tulioutaja na sio katika mas'ala ya imani na itikadi.

Ama kuhusu yale yanayochochewa kwamba watu wa dini nyingine wana maswali juu ya dini yetu, maswali haya yapo nayo hayafungamani na mas'ala ya kuleta mwafaka wala hayafungamani na mas'ala ya uwazi, bali yanafungamana na upeo wa ijtihadi yetu katika kutoa majibu juu ya maswali haya ambayo yanatolewa dhidi ya dini yetu na itikadi yetu. Na tangu zamani kulikuwa na maswali yaliyokuwayanatolewa hata kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Na vilevile katika wakati wa Maimamu (as) yalikuwa yanaulizwa maswali juu ya sharia ya Kislamu na juu ya nadharia ya Kiislamu, na Maimamu (as) walikuwa wanayajibu.

Maudhui ya kumuuwa mwenye kuritadi ni swali pana na ni lenye kuulizwa, na mafaqihi wanayo majibu. Katika mfano wa misimamo hii sisi tunatoa majibu yetu na hatulazimiki kuuridhisha upande wa pili ambao unaweza kukinai au kutokinai, nao uko huru katika hilo. Lakini ni juu yake kuheshimu rai yetu. Na kuhusu mas'ala ya kumuuwa mwenye kuritadi kuna maneno na mijadala, na kuna baadhi

ya rai humo zenye mjadala kuhusu hukumu hii, na lililo mashuhuri kwa mafaqihi ni rai hii (ya kumuuwa murtadi).

Na vilevile kuhusu kuingia kafiri Makka na kuoa kwake mwanamke Mwislamu hii haijuzu kisharia, na upande mwingine unapouliza sisi tunajitahidi kumkinaisha kwa mtazamo wetu, na kama hatokinai sio lazima kwetu kumkinaisha. Kama ambavyo sisi pia tuna maswali kuhusu Wahindu, Mayahudi na Manaswara, na sisi hatukinaiki na rai zao, na sio sharti tukinai na rai zao au wao wakinai kwa rai zetu, lakini ni wajibu kuwepo na kuheshimiana. Uwazi haumaanishi kwamba upande huu ukubali rai ya upande mwingine au ukinai na sababu zao, uwazi unamaanisha kufahamu sababu za upande mwingine na kumheshimu mwingine na kushirikiana katika maslahi yenye kuwashirikisha pamoja, hii ndio maana ya uwazi.

**Sayyid Muhammad Da'aluj:**

Tunatanguliza shukurani za dhati, swali ambalo linazunguka katika akili za watu wengi: Ni je, kuna tofauti baina ya uwazi na kuleta ukaribu baina ya madhehebu? Vilevile je, uwazi unahusiana tu na itikadi na madhehebu au kuna mambo mengine ni wajibu kuyazungumzia zaidi kuliko kusisitiza juu ya ikhitilafu za kimadhehebu katika harakati za uwazi? Na nina mchango kuhusu Sheikh kuigawa jamii makundi mawili katika yanayohusu maudhui ya uwazi, kwamba kuna anayeufanyia kazi uwazi na ni mwenye kuamini katika hilo, na kuna mtu mwingine ambaye mmesema kwamba yeye haungi mkono uwazi, ambapo mimi naona kwamba kuna sehemu nyingine (ya tatu) nayo ni yule aliye dhidi ya fikira hii, yeye anaipinga kwa nguvu fikira hii. Kuna wakati yanapatikana mazungumzo juu ya uwazi na kuleta ukaribu baina ya madhehebu, lakini hayapatikani mazungumzo kuhusu malengo na mafanikio yaliyotokana na baadhi ya harakati za uwazi na kuleta ukaribu ili yawe ni kiungo kwa msikilizaji.

**Sheikh Safar:**

Uwazi na kuleta ukaribu zinaweza kuwa ni anwani mbili zinazokaribiana zenye kuingiliana kama nilivyoashiria, lakini tukitaka kupambanua baina ya misemo hii uwazi ni hatua tunayoanza nayo, nayo ni kuuelewa na kuujua upande mwingine na kuleta uhusiano pamoja nao, wakati ambapo kuleta ukaribu ni juhudi za kupata sehemu za ushirikiano na kujaribu kupanga maslahi ya pamoja baina ya pande hizi.

Ama nukta ya pili ambayo mmeizungumzia nayo ni nukta muhimu, kwamba mas'ala sio mas'ala ya uwazi wa kiitikadi na kifikira tu, lakini kinachotakiwa ni kuwepo na uwazi wa kijamii na kivitendo kwa kutengeneza miradi ya pamoja. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba unakaribia kuwepo utengano wa kimadhehebu au wa kikanda hata katika kazi za kibinadamu, kiasi kwamba kunapatikana wanaosaidia mafakiri wa kishia tu katika nchi hii, na hawana uhusiano na mafakiri wa kisunni, na vile vile kuna wanaosaidia mafakiri wa kisunni tu na hawana uhusiano na mafakiri wa kishia. Hata kuoleana baina ya watu wa madhehebu kunahesabiwa kuwa ni dhamana ya umoja na kuleta ukaribu, kwa sababu kuwepo hali ya kuoleana kunasaidia kuamiliana na kujuana ndani ya nyumba. Na katika hali hii propaganda na uvumi havitokubalika. Katika nchi ambazo kunapatikana hali ya kuoleana bila kujali madhehebu hali ya watu katika kuamilina na kuleta ukaribu ni bora zaidi.

Nukta ya mwisho ambayo mmeiashiria, nayo ni kwamba mas'ala sio ni nani analingania katika kuleta ukaribu na ni nani asiyefanya hivyo, lakini kuna anayefanya kazi dhidi ya uwazi na dhidi ya kuleta ukaribu. Hapa ni wajibu niseme kwamba kwa masikitiko makubwa kuna baadhi ya sauti au baadhi ya pande – na nataraji zisiwe zinasukumwa na ushindani wa kijamii wa ndani dhidi ya nguvu zingine, na wala zisiwe zinasukumwa na changamoto ya kutaka kuthibitisha

uwepo wa vitu – ambazo zinaweza kusababisha madhara juu ya maslahi ya jamii na mustakbali wa madhehebu kwa sababu tu ya uadui binafsi. Kadhia ni kwamba sio ushujaa au ujasiri kusema wazi rai inayoamsha hisia za upande mwingine. Mimi nalingania utulivu na kurejea katika maneno ya Ahlulbayt (as) kiasi kwamba Hadithi za Ahlulbayt (as) katika Taqiya ni nyingi, na amesema Imamu as-Sadiq (as): "Hakika Taqiya ni dini yangu na ni dini ya wahenga zangu. Na hakuna dini kwa asiyekuwa na Taqiya."[16] Na "Tisa ya kumi (9/10) ya dini ni katika Taqiya."[17]

Taqiya maana yake ni pana, na miongoni mwa maana zake ni upendo na kuamiliana vizuri na wengine. Wako wapi hawa na nususi hizi na Hadith? Kwa nini wanatafuta riwaya fulani au ziyara fulani na wanazinyanyua kuwa ndio bendera, na wanaghafilika na maelfu ya Hadithi ambazo zinazungumzia juu ya Taqiya na muamala mwema na asili ya muamala mzuri. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Msiwasimulie watu yale ambayo hamyajui."[18] Na kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) amesema: "Kuweni ni pambo kwetu na wala msiwe ni dosari kwetu. Tupendezesheni kwa watu na wala msituchukize kwao. Vutieni kwetu kila upendo na epusheni kwetu kila shari."[19] Na kutoka kwaUmar bin Ibaana amesema: Nilimsikia Abu Abdillah (as) anasema: "Enyi Shia, hakika nyinyi mmenasibishwa kwetu, hivyo kuweni pambo kwetu na wala msiwe ni dosari, kuweni mfano wa wafuasi wa Ali (as) katika watu. Ikiwa mtu miongoni mwao (Shia) yuko katika kabila basi awe imamu wao na mwadhini wao, mtunza amana zao na sehemu yakuweka vitu vyao. Tembeleeni wagonjwa wao na shuhudieni jeneza

[16] Al-Hurrul-A'miliy: Muhammad bin Hasan katika *Wasa'ilu-Shi'ah*, Juz. 16, uk. 210 Hadithi 21379, Chapa 1 mwaka 1993, Muasasatu Aal Bait lil Ihiyaai Turathi- Beirt

[17] *Al-Kaafiy*, Juz. 2, uk. 217 Hadith 7.

[18] *Biharul-An'war*, Juz. 2, uk. 77 Hadith 61.

[19] *Wasa'ilu-Shi'ah*, Juz. 12, uk. 8 Hadith 15502.

zao na swalini katika misikiti yao na wala wasiwatangulieni katika kheri, nyinyi Wallahi mna haki zaidi kwayo kuliko wao."[20]

Kutoka kwa ImamuAli (as) amesema: "Wasimulieni watu yale wanayoyajua na jizuieni na yale ambayo wanayakataa." Na kutoka kwake (as) amesema: "Mwenyezi Mungu amrehemu mja anayevutia mapenzi ya watu katika nafsi yake na kwetu, kwa kudhihirisha kwao wanayoyajua na kwa kuwaepusha na wanayoyakataa."[21] Inakuwaje wanaruhusu katika nafsi zao kughafilika na nususi hizi – ambazo ni mamia au maelfu - kwa ajili ya maslahi ya nasu ambayo kuna maneno juu ya kuthibiti kwake na usahihi wake?

Hebu tuvuke maudhui ya nususi na tutazame uhalisia wa nje wa muamala, tutazame tunaishi katika hali gani. Kuna kundi linashambulia ukanda huu, na njama zinawatishia wananchi wa ukanda huu. Wamarekani na njama zao, Mazayuni na uadui wao, na Magaidi na wakufurishaji na nafasi yao. Kisha sisi tunakuja ili tuweke chumvi katika jeraha na tunamwaga mafuta kwenye moto. Hawa ni wajibu wao kutazama upya, mimi situhumu nia ya yeyote wala sitii shaka katika dini ya yeyote.

Nimekumbuka swali alilouliza ndugu yangu, anasema: Nyinyi mnawatuhumu wengine kwamba wao wanafanya ugaidi wa kifikira kwa jina la kuhami itikadi, je na nyinyi mnafanya ugaidi wa kifikira? Kwa hakika ugaidi wa kifikira ni kutia shaka katika diniya mwingine na kumtuhumu na kujaribu kumwangusha kijamii. Sisi tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuweke mbali na vitendo hivi. Hatujatoa fatwa ya kumkufurisha yeyote na hatujatoa tamko la kutia shaka dini ya yeyote. Madhumuni ni kwamba sisi tunashikamana na haki yetu katika kutoa rai zetu na tunakataa kupokonywa haki hii, na wengine wanatoa rai zao na wao wako huru. Lakini kwa masikitiko makubwa kuna watu

[20] *Biharul-An'war*, Juz. 85, uk. 119.
[21] Biharul-An'war, Juz.2, uk.77.

ambao wanaona maneno yao kuwa ni asili na sharia, na maneno mengine yoyote yako nje ya sharia na wala haisihi kusemwa. Sisi tunakataa wala hatukubali yeyote kujimilikisha uhalali wa kubainisha sharia au yeyote kutukandamiza katika suala la kubainisha sharia. Alhamdulillahi, sote tumesoma katika madrasa ya Ahlulbayt (as) na tumechota katika maarifa yao na kila upande unarejea zake, tegemeo lake, hoja zake na dalili zake.

Hakika kuna watu ni wajibu wao watafakari na watazame upya je, maneno haya makali ambayo wanayatoa mbele ya mwingine, je yanaafikiana na idadi hii kubwa ya riwaya za Ahlulbayt (as) na nususi zao. Je yanaafikiana na sira ya Ahlulbayt (as), je wewe unajali zaidi madhehebu kuliko Maimamu wenyewe wa madhehebu? Maimamu wa madhehebu hawakusema maneno haya na kwa njia hii. Na hata tukifumbia macho yote hayo, wewe unaishi katika hali gani? Na unaishi katika zama gani? Je, huoni mazingira yanayokuzunguka? Ni lazima mambo haya yafanyiwe hesabu?

ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعۡلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Surat Nahli: 125).**

Na hekima ni kuweka mambo katika mahala pake.

Hakika mimi nailingania nafsi yangu na ndugu zangu miongoni mwa maulamaa, makhatibu na wenye kujali mambo ya ummah, tusitende kwa msukumo wa changamoto za kuhasimiana sisi kwa sisi. Hii inadhuru maslahi ya jamii, changamoto na ukaidi unapelekea

kwenye vitu vinavyonidhuru mimi na kukudhuru wewe na vinawadhuru wote. Vinadhuru madhehebu na nchi kwa ujumla. Tunapohitalifiana katika rai ni juu yetu tuhukumiane kwa dalili na hoja na kwa uhuru wa kutoa rai, kutoa badali, na kwa kuheshimiana. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwafikishe sote katika kheri na kuamiliana vizuri na wengine.

**Alhaji Hasan Faraj:**

Tunamshukuru Sheikh kwa muhadhara huu mzuri ambao tunataraji utafuatiwa na mingine mfano wake, ili tuwaelimishe vijana wetu na watoto wetu kwa utamaduni wa uwazi na kupeana na wengine.

**Mwenyekitiwa semina:**

Ni mwishoni mwa semina hii, hatuna tena wakati isipokuwa kumshukuru Muadham Sheikh Hasan Musa Safar, na tunawashukuru nyote kwa kuhudhuria kwenu.

**Wasalamu Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuhu.**

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashariyyah
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala

16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)

37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah

78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Huduma ya Afya katika Uislamu
97. Sunan an-Nabii
98. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)

99. Shahiid Mfiadini
100. Ujumbe - Sehemu ya Kwanza
101. Ujumbe - Sehemu ya Pili
102. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
103. Ujumbe - Sehemu ya Nne
104. Kumswalia Nabii (s.a.w)
105. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
106. Hadithi ya Thaqalain
107. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
108. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
109. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
112. Safari ya kuifuata Nuru
113. Fatima al-Zahra
114. Myahudi wa Kimataifa
115. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
116. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
117. Muhadhara wa Maulamaa
118. Mwanadamu na Mustakabali wake
119. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)

120. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
121. Khairul Bariyyah
122. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
123. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
124. Yafaayo kijamii
125. Tabaruku
126. Taqiyya
127. Vikao vya furaha
128. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
129. Visa vya wachamungu
130. Falsafa ya Dini
131. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
132. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
133. Kuonekana kwa Allah
134. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
135. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
136. Ushia ndani ya Usunni
137. Maswali na Majibu
138. Mafunzo ya hukmu za ibada
139. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
140. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2

141. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
142. Abu Huraira
143. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
144. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
145. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
146. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
147. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
148. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
149. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
150. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
151. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
152. Uislamu Safi
153. Majlisi za Imam Husein Majumbani
154. Uislam wa Shia
155. Amali za Makka
156. Amali za Madina
157. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
158. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
159. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
160. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
161. Umoja wa Kiislamu na Furaha

162. Mas'ala ya Kifiqhi
163. Jifunze kusoma Qur'ani
164. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
165. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
166. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
167. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
168. Uadilifu katika Uislamu
169. Mahdi katika Sunna
170. Kazi naBidii ni njia ya maendeleo
171. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
172. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
173. Vijana naMatarajio ya Baadaye
174. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
175. Ushia – Hoja na Majibu
176. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
177. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
178. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
179. Takwa
180. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
181. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a.s.)

182. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
183. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
184. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
185. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
186. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a.s.)
187. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii
188. Huduma ya Afya katika Uislamu
189. Historian a Sira za Viongozi Waongofu – Sehemu ya Pili
190. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# MUHTASARI

# MUHTASARI

# MUHTASARI

## MUHTASARI